

**TUME YA
KUREKEBISHA
SHERIA TANZANIA**



USAJILI WA NDOA

5.3 Kimila

Ndoa hizi zinazofungwa kwa kufuata taratibu za kabila husika ambalo wanandoa wanatoka. Ni wajibu wa afisa msajili aliyehudhuria ndoa kuisajili ndoa hiyo. Endapo ndoa imefungwa bila ya uwepo wa afisa msajili, ni wajibu wa wahusika kuomba usajili, katika kipindi cha siku thelathini baada ya ndoa kufungwa.

6.0 FAIDA ZA KUSAJILI NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya Ndoa, kila ndoa iliyofungwa iwe ya kidini, kiserikali au kimila inapaswa isajiliwe kwenye daftari la Msajili Mkuu wa Ndoa. Usajili wa ndoa una faida zifuatazo: kurahisisha taratibu katika mashauri yanayohusu talaka na mirathi kwa kuwa cheti ni ushahidi wa ndoa husika; kutambua wamiliki wa mali za wanandoa; Serikali kuwa na kumbukumbu sahihi za ndoa zinazofungwa nchini.

8.0 HITIMISHO

Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo ni msingi wa upangaji wa maendeleo ya nchi katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :

**Katibu Mtendaji,
Tume ya kurekebisha Sheria
Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA
TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz**

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. kwa mujibu wa sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitekinolojia. Tume imefanya Mapitio ya Sheria zinazohusu Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu 2017.

2.0 SHERIA YA NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yote.

3.0 VIGEZO VYA KUZINGATIWA

Vigezo vya msingi vya kuzingatia ili kufanya muungano huo (ndoa) utambulike kisheria ni vifuatavyo:

3.1 HIARI:

Muunganiko huo ni lazima utokane na ridhaa ya wahusika wenyewe; pasipo udanganyifu, au ulaghai wa aina yoyote:

3.2 KUSUDIO LA KUDUMU

Muunganiko wa wanandoa sharti uwe umekusudiwa kuwa kudumu, isipokuwa kama litatokea jambo ambalo ni nje ya uwezo wa wanandoa kama vile kifo cha mmoja, ndoa kukumbwa na matatizo kisha talaka kutolewa.

3.3 Jinsi tofauti

Ndoa sharti iwe kati ya Mwanume na mwanamke, watu wenye maumbile tofauti ya via vya uzazi.

3.4 Isihusishe Maharimu:

Maharimu ni watu walio na mahusiano ya karibu ya damu au kindugu, Sheria inazuia ndoa kati ya dada na kaka, baba na binti yake, mama na mwanawe, babu au bibi na mjukuu wake, shangazi au mjomba na mpwawe, au baba ama mama mlezi na mtoto aliyemuasili.

3.5 Umri:

Kigoze cha umri kimetajwa katika muktadha tofauti tofauti, lakini kwa ujumla, wanandoa wanapaswa kuwa na umri wa miaka 18 au ziaidi.

3.6 Kusiwe na Ndoa inayoendelea.

Kama mwanamke ana ndoa inayoendelea na kutambulika kisheria haruhusiwi kufunga ndoa nyingine. Vilevile, kama mwanume ana ndoa ya mke mmoja au ni muislam ana wake wanne hataruhusiwa kufunga tena ndoa nyingine.

3.7 Kusiwe na Pingamizi:

Kabla ya ndoa kufungwa ni lazima tangazo litolewe juu ya kusudio la kufunga ndoa, na ndoa haitafungwa endapo kutakuwa na pingamizi halali kutoka kwa mtu mwenye haki ya kufanya hivyo.

3.8 Mamlaka ya kufungisha ndoa (Mfungishaji ndoa awe na mamlaka ya kufanya hivyo):

Mfungishaji wa ndoa ni lazima awe na leseni ya kufungisha ndoa kutoka kwa Msajili Mkuu wa Ndoa. Ndoa inayofungwa na mtu asiyepa leseni ni batili.

3.9 Mashahidi: Ndoa ni lazima ishudiwe na mashahidi wasiopungua wawili wenye umri usio chini ya miaka 18 na mwenye akili timamu na kuelewa lugha inayotumika katika ufungishaji ndoa.

3.10 Wafunga ndoa wote wawili wawepo:

Wanandoa wote wawili sharti wawepo wakati wa tukio la kufunga ndoa. Hata hivyo, sheria inaruhusu ndoa kufungwa ikiwa mmoja wa wafunga ndoa hayupo lakini amewakilishwa na mtu ambaye anakuwepo wakati wa kufungwa kwa ndoa.

4.0 AINA ZA NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ndoa, kuna aina mbili za ndoa zinazotambulika, nazo ni ndoa ya mke mmoja na ndoa ya wake wengi.

5.0 UFUNGISHAJI NA USAJILI WA NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 (1) cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, kuna aina tatu za ufungishaji ndoa ambazo ni :

5.1 Kidini

Noda zinazofungishwa kidini hufuata taratibu za dini husika ambayo wanaandaa ni waumini. Ndoa ikifungishwa kidini, ni wajibu wa kiongozi wa diini husika kuisajili ndoa hiyo harka iwezekanavyo.

5.2 Kiserikali

Ndoa zinazofungishwa na Mkuu wa Wilaya za zimekuwa zikifahmika kama "ndoa za bomani." ni wajibu wa msajili wa Wilaya kusajili ndoa hiyo.